

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



S.L.P 42325,
Simu Nambari: 2850633
Nukushi: (022) 2850635
Barua Pepe: rbctemeke@pccb.go.tz
Wavuti: www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

TEMEKE 30/06/2020

MHARIRI WA MAGAZETI YA SERIKALI AKAMATWA KWA RUSHWA

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Temeke jijini Dar Es Salaam, imemkamata Mhariri wa Magazeti ya Serikali kwa kosa ya kuomba na kupokea Rushwa kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11/2007.

Uchunguzi wa TAKUKURU ulibaini kwamba, mnamo tarehe 29/06/2020 OSCA JOSEPH MBUZA ambaye alijitambulisha kuwa ni Mhariri wa Magazeti ya Serikali, awali akiwa katika kampuni inayoshughulika na utengenezaji wa Nondo aliomba fedha Dolla 6,000 za Kimarekani na baadaye alibadili na kutaka kiasi cha shilingi 5,000,000/= na hatimaye alipokea fedha za mtego kiasi cha Shilingi 1,500,000/= ili aweze kuficha kuwa kampuni hiyo (jina limehifadhiwa) kuwa na mfanyakazi raia wa kigeni anayefanya kazi nchini pasipo kuwa na kibali cha kufanya kazi na cha kuishi nchini.

Uchunguzi dhidi ya tuhuma hii umekamilika na mtuhumiwa anatarajiwa kufikishwa mahakamani leo Jumanne Juni 30, 2020 na kufunguliwa mashitaka kwa kosa la kushawishi, kuomba na kupokea rushwa kinyume na Kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11 ya mwaka 2007, katika Mahakama ya Wilaya ya Temeke.

TAKUKURU Mkoa wa Temeke inatoa wito kwa wananchi wote kuendelea kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kupitia mitandao yote ya simu kwa kupiga au kutuma ujumbe mfupi kwa namba ya bure 113 au kupiga 113 au kufuata maelekezo au fika katika ofisi ya TAKUKURU iliyopo karibu nawe.

JENGA NCHI YAKO KATAA RUSHWA

Imetolewa na:

Donasian Kessy

Mkuu wa TAKUKURU (M)

Temeke